Swahili

Year 7

**MARCH EXAMINATION 2021** **1 hr. 30 min**

Additional Materials:

Soft clean eraser
Soft pencil (type B or HB recommended)

***Read these instructions first***

This paper contains 4 sections Answer all questions in the spaces provided.

Do **not** use staples, paper clips, and glue or correction fluid.

Any rough working should be done in the rough work booklet provided.

NAME**:** …… DATE: ……

SCORE:

TOTAL MARKS:

## 1.Kusoma

# SAMAKI CHAKULA BORA

Ni kiumbe Cha majini, hakidumu aridhini,

Huishi chini kwa chini, uhai wake rnajini,

Mtoni au baharini, kidirnbwini au ziwani,

Humo huwa burudani, samaki yu furahani,

Vsijifanye kuhani, kwenda mtoa bwawani,

Kula uujenge mwili, samaki chakula bora.

Samaki kuogelea, raha mwake maishani,

Mayai yanaelea, watoto toka turnboni,

Huangua kuenea, wengineo duniani,

Hawana haja kulea, chakula chao maiim,

Hula pia na mimea, kila siku wa mbioni,

Kula uujenge mwili, samaki chakula bora.

Samaki ni kitoweo, kitamu mwako kinywani,

Hata kwa wageni wako, wajapo kwako nyumbani,

Talamba vidole vyao, akipikwa kwa makini,

Kiboma pia aweko, ladha yake ina shani,

Pono naye akiwepo, minofuye ni Iaini,

Kula uujenge mwili, samaki chakula bora.

Ngui naye simuche, japo ataka makini,

Uchafu wake upae, mtie kikaangoni,

Muache huko akae, moto uingie ndani.

Mfunike kwa kigae, akaukie ndani,

Limau mnyunyizie, mwisho aje sahanini,

Kula uujenge mwili, samaki chakula bora

Porotini utapata, unapokula samaki,

Kula tafi hutajuta, utaondoa hamaki,

jodari hana utata, na changu aso mikiki,

Mkaange kwa mafuta, au nazi bila chuki,

Minofu kama ya mbuta, mle huhofu huchoki,

Kula uujenge mwili, samaki chakula bora.

(Kwa mashairi mengine, soma Nachora kwa Maneno, na Swaleh Mdoe, OUPEA.)

## Jibu maswali yafuatayo.

1. Shairi hili ni la aina gani? Alama 2

……

2.Shairi hili linazungumzia nini? Alama 2

……..

3. Sentensi gani si sahihi? Alama 1

A. Samaki huishi baharini.

B. Samaki huishi katika nchi

C. Samaki huishi ziwani.

D. Samaki huishi kidimbwini.

4. Vina vya ubeti wa mwisho katika shairi hili ni Alama 2

……

5. Mshororo wa kwanza wa shairi hili una mizani ngapi? Alama 2

……

6. Samaki hutupatia aina gani ya madini? Alama 1

a. Porotini

B. Kabohaidreti

C. Vitamini

D. chuma

7. Kauli: Ladha yake ina shani. ina maana kuwa? Alama 1

A. ladha ya samaki ina tuzo ya nishani.

B. samaki ana ladha ya ajabu na inayovutia.

C samaki ana ladha isiyopendeza.

D. samaki ana ladha inayochukiza.

8. Taja kiungo kinachotiwa kwa kitoweo cha samaki kulingana na shairi. Alama 1

A. Limau

B. Karafuu

C. Kitunguu

D. Pilipili

9. Samaki yupi huhitaji maarifa kupika? Alama 1

A. Kiboma

B. Jodari

C. Ngisi

D. Pono.

10. Andika kibwagizo cha shairi hili. Alama 2

……

## 2. SARUFI

A. Kamilisha sentensi hizi kwa neno sahihi kati ya yale uliyopewa. (Alama 5)

1. ---------- haya ni ya ---------- yule. (maskini/maskani)

2. Hamali huyu anafanya---------- yake kwa----------. (kazi/kasi)

3----------alienda baharini akamvua---------- mkubwa sana. (papa/baba)

4. Mara tu walipo_____ daraja moshi ulianza ku_____. (vuka/fuka)

5. Wauguzi walikuwa waki_____ na walipo_____, tayari madhara yalikuwa yametendeka. (koma/goma)

B. Tumia -Ote kwa njia sahihi kukamilisha sentensi. ( Alama 5)

l. Ukuta_____ umebomoka.

2. Daraja_____ limeharibika.

3. Mihandarati_____ ilipigwa marafuku.

4. Mahali_____ mmejaa maji.

5. Makala_____ yalipigwa chapa.

.

C. Andika sentensi hizi katika umoja (Alama 5)

1.Barabara zote zimejaa takataka.

_____

2.Mikate mitamu iliokwa na wapishi hawa.

_____

3.Makabati yote yalifanyiwa ukarabati.

_____

4.Wagonjwa wote wamepata matibabu.

_____

5.Kutembea kwote kulituchosha sana.

_____

ANDIKA AINA TANO ZA RANGI. (Alama 5)

1._____

2._____

3. _____

4._____

5._____

Andika majina ya nambari zifuatazo. (Alama 5)

1. 53- _____

2. 47-_____

3. 124-_____

4.69-_____

5. 1268-_____

# 4. MSAMIATI.

A. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Kuku ni aina ya ndege anayefugwa nyumbani. Kuku hupenda kukaa vichakoni au kwenye vivuli vya miti. Hawapendelei jua kali au baridi kali. Baridi kali hupunguza uwezo wao wa kutaga na pia huwapa magonjwa.

Kinyesi cha kuku ni mbolea ya hali ya juu. Mkulima anayefuga kuku mia moja anaweza kupata tani mbili za mbolea kwa mwaka. Mbolea hii huwa ni mchanganyiko wa kinyesi cha kuku na taka wanazowekewa sakafuni.

Kuna aina mbili za kuku, wa kigeni na wa kienyeji. Kuku wa kienyeji hufika uzito wa kilo moja na nusu wakiwa na umri wa wiki ishirini na moja. Kuku wa kigeni nao hufikia uzito huo wakiwa na wiki nane pekee.

l. Kifungu hiki kina aya ngapi? Alama 1

_____

2. Taja idadi ya sentensi katika kifungu hiki. Alama 3

_____

3. Sentensi ya kwanza katika aya ya kwanza ina maneno mangapi? Alama 2

_____

4. Maneno yafuatayo yana silabi ngapi? Alama 5

(a) vichakani-_____

(b) kinyesi-_____

(c) kiwanda-_____

(d) changanyiko-_____

(e) wanazowekewa-_____

5. Neno mkulima lina herufi ngapi za konsonanti? Ziandike. Alama 2

---

B. Jaza mapengo kwa majibu sahihi. Alama 5

I . Watu wanapoagana husema _____

2. Mtu anapomtembelea mwingine. hubisha kwa kusema_____

3. Watu wanapoenda kulala huambiana_____

4. Wadogo huwaamkia wakubwa zao kwa kusema_____

5. Majibu ya masalkheri ni_____

C. Andika sentensi zifuatazo kwa kutumia msamiati mwafaka wa heshima. Alama 3s

1. Musa tafadhali _____ nakala yako ya Kiswahili Sanifu.

2. Maskinil Ni kweti kuwa mlezi wake _____

3. Alipopatwa na kipindupindu _____ na kutapika.

# 4. KUANDIKA (Alama 20)

A. Yapange maneno haya vizuri ili kuunda sentensi sahihi. Alama 10

I. Ishara ni heshima ya maamkizi.

_____

2. Ilipendeza wakati niliyohudhuria likizo sherehe sana wa.

_____

3. Asubuhi ya sababalheri maamkizi ni

_____

4.Wakubwa husglimia wanapokutana wadogo ndio.

_____

5.. Bi njiani Kizito na nilikutana.

_____

B.Andika insha fupi kuhusu rafiki yako. Alama 10

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……